

FOLD

FOLD

Je, simu za mkono ni salama?

Utafiti wa sasa wa kisayansi haujagundua ithibati zozote zinazopendekeza kwamba matumizi ya simu ya mkono (ndani ya mipaka iliyowekwa na viwango vya kimataifa) yanaweza kuwa na athari mbaya kwa afya ya binadamu - hata katika hali ya hatari ya muda mrefu.

Habari zaidi kuhusu viwango vya SAR?

Watumiaji wanaotaka kupata taarifa maalum kuhusu viwango vya SAR vya simu zilizopo wanapaswa kuwasiliana na Jukwaa la Watengenezaji wa Simu (MMF): www.mmfa.org. Shirika la kimataifa lisilo la kiserikali lililoanzishwa mnamo 1998 na watengenezaji kadhaa wa vifaa vinavyotumia masafa ya mawasiliano (ikijumuisha Nokia, Erikson, Mitsubishi Electric, Motorola, Nokia, Panasonic, Philips, Sagem, Samsung, Nokia, Sony Erikson na TCL) , Jukwaa la Watengenezaji wa Simu hutoa fedha za utafiti wa matumizi ya simu ya mkono na afya ya binadamu, ushirikiano/Uratibu wa viwango na masuala ya kisheria (hususani pamoja na Mradi wa uga wa Kawi ya sumaku ya kielektroniki ya WHO), na huwa jukwaa la mawasiliano ya umma kwa ujumla.

Je, ni salama kuishi karibu sana na Minara ya Mawasiliano ya Simu ? Hakuna athari mbaya za kiafya zilizotambuliwa kuathiri watu wanaoishi karibu na Mnara wa Mawasiliano ya Simu. Huku watu wengine wakiwa wameripoti udhihirisho wa dalili zisizo maalum kama matokeo ya hatari ya mionzi ya nguvu ya sumaku umeme inayotokana na Minara ya Mawasiliano ya Simu kuwapo kwa hatari ya nguvu ya sumaku umeme kwa vijenzi vya mwili haijathibitishwa kuwa sababu ya dalili kama hizo. Antena ya Minara ya Mawasiliano ya Simu (kawaida iliyowekwa kwa majengo au minara kwa urefu wa mita 15 hadi 50 juu ya ardhi) hutoa miale miembamba ambayo hupungua kwa kiwango cha uelekeo wa masafa ya mtumiaji wa simu ya mkono kutoka kwa Mnara wa Mawasiliano ya Simu. Sehemu ambayo miale inashikana na ardhi pia ni ya chini kiasi cha kufanya nguvu zake ziwe chini sana kuliko ile ya mionzi iliyopendekezwa.

Je, ni sheria zipi zinazoshughulikia uwekaji wa mtambo wa mawasiliano?

Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya, kwa kushirikiana na washirika wote wanaohusika, kwa sasa iko katika mchakato wa kuunda 'Kanuni ya Utendaji wa Uwekaji wa Minara ya Mawasiliano ambayo itashughulikia hofu zozote zilizowasilishwa na wale wanaoishi karibu na Minara ya Mawasiliano ya Simu . Ingawa utafiti wa kisayansi umebainisha kuwa mionzi yote hiyo inatolewa kwa mipaka salama, kanuni hii itashughulikia masuala kama; usawa wa uafikiaji na mitandao mbalimbali na hitaji la usikivu katika eneo la Minara ya Mawasiliano ya Simu .

Kwa habari zaidi kuhusu RF/EME na afya ya binadamu, tazama yafuatayo:

1. Wavuti wa Shirika la Afya Duniani: www.who.int
2. Miongozo ya ICNIRP: www.icnirp.de/documents_emfgdl.pdf

Unahitaji kufahamu zaidi?

Kwa habari zaidi kuhusu mada iliyopo hapo juu au sehemu nyingine yoyote ya afya na usalama wa mitambo ya mawasiliano, tafadhali wasiliana na:



Head Office

CA Centre, Waiyaki Way, P.O. Box 14448, Nairobi 00800
Mobile: 0703042000,
Talk to us: pea@ca.go.ke | chukuahatua@ca.go.ke
020-445 5555, 0714 455 555, 0737 455 555

CA Western Regional Office

1st Floor KVDA Plaza
P.O. Box 2346
Eldoret 30100
Mobile: 0703042105
Email: wro@ca.go.ke

CA Coast Regional Office

3rd Floor, NSSF Building
P.O. Box 8041
Mombasa 80100
Mobile: 0703042152
Email: cro@ca.go.ke

Central Regional Office

Ground Floor, Advocates
Plaza
P.O. Box 134
Nyeri 10100
Mobile: 0703042181
Email: cero@ca.go.ke

Nyanza Regional Office

2nd Floor Lake Basin Mall,
P.O Box 2016
Kisumu 40100
Mobile: 0703042130
Email: nro@ca.go.ke

Ilani ya kujitoa hatarini: Huku kila jaribio likiwa limefanywa ili kuhakikisha kuwa habari iliyojumuishwa katika hati hii ni sahihi, imekusudiwa TU kuwa kama mwongozo wa kuelekeza utendakazi salama wa mitambo ya mawasiliano na haipaswi kuchukuliwa kama (au kutumika badala ya) ushauri wa kisheria. Kwa hivyo, Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya haitakubali kosa lolote kwa matokeo ya hatua zozote zilizochukuliwa, au maamuzi yaliyotolewa kwa misingi ya taarifa iliyotolewa.

CA/PEA/CEP/KIS/B/2/2020



www.ca.go.ke

**NGUVU YA SUMAKU
UMEME NA AFYA
YA BINADAMU**



FOLD

FOLD



Kipeperushi hiki kimetayarishwa kama sehemu ya Programu ya Elimu ya Watumiaji ya Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya. Kiliandaliwa pamoja kama matokeo ya ukaguzi wa nyaraka kutoka kwa vyanzo mbalimbali na inawasilisha mtazamo wa sasa wa habari iliyoko kuhusu athari za nguvu ya sumaku umeme kwa afya ya binadamu.

Utangulizi

Matumizi ya simu za mkono nchini Kenya yanaongezeka sana nchini Kenya. Kwa sababu hiyo, kumekuwa na ongezeko la nia kutoka kwa umma inayohusu masuala ya kiafya yanayohusiana na kuhatarisha wanadamu kwa mionzi ya Nguvu ya Sumaku Umeme (EMF).

Je, kiwango cha masafa ya nguvu ya sumaku umeme ni kipi (RF/EME) Simu za mkono pamoja na Minara ya Mawasiliano ya Simu (BTS) hutoa Masafa ya Umeme (RF) ya Nguvu ya Sumaku Umeme (EME), ikiwa ni aina ya mionzi ambayo inajulikana kama Mionzi Isiyo na Madhara (NIR) – kwa sababu haiwezi kubadilisha muundo wa masi. Mionzi iliyo na madhara (kama vile mionzi ya uyoka na Mionzi ya Gamma), kwa upande mwingine, ina uwezo wa kusababisha madhara (mnunuriko) na kusababisha mabadiliko ya chembechembe za mwili, ambayo mengine yanaweza kuharibu vijenzi vya mwili wa binadamu.

Vyanzo vya masafa ya mionzi ya nguvu ya sumaku umeme vinavyozalishwa na binadamu vinajumuisha:

- Simu za mkono na Minara ya Mawasiliano ya Simu (BTS)
- Vidhibitumbali
- Vipeperushi vya matangazo
- Vifaa vya umeme na kielektroniki

Kiwango cha hatari kinachosababisha RF/EME ambacho mtumiaji wa simu ya mkono hupata kinategemea pakubwa: idadi na muda wa simu zinazopigwa, kiasi cha simu ya mkono zinazopigwa kwa wakati mmoja, umbali wa mtumiaji kutoka kwa Minara ya Mawasiliano ya Simu ilivyo karibu, ubora wa upeperushaji, umbali wa antena, na ukubwa wa simu ya mkono. Chanzo kikuu cha RF/EME cha simu ya mkono kiko katika

antena yake, ambayo iko katika simu yenyewe. Kwa kuwa simu yenyewe kwa kawaida inashikwa pembeni mwa kichwa pale inapotumika, kadri antena hiyo inavyokaribia kichwa, ndivyo hatari ya nguvu ya sumaku umeme unavyozidi.

Utafiti wa kina unaendelea kufanywa kwa madhumuni ya kutathmini hatari zilizopo kwa binadamu kutokana na hatari ya RF/EME. Utafiti uliofanywa na jamii ya kimataifa ya wanasayansi kufikia sasa, hata hivyo, umebaini kuwa hatari ya muda mrefu na RF/EME inaweza, katika hali fulani, kusababisha joto jingi kwa vijenzi vya mwili, mshtuko na kuchomwa kutokana na vifaa na msimko wa misuli na neva, viwango vya hatari ambavyo umma unavyo kwa sasa viko chini ya viwango vinavyohitajika ili kusababisha athari mbaya za kiafya (takriban mara 100 chini ya viwango hivyo).

Ni taasisi gani inayodhibiti - RF/ EME?

Utoaji wa mionzi inayodhuru unadhibitiwa nchini Kenya na Bodi ya Ulinzi wa Mionzi (RPB). Kwa wakati huu, Bodi hii haina wajibu wa kudhibiti utoaji wa RF/EME. Hata hivyo, mswada wa bunge sasa unaandaliwa, ambao hatimaye utatoa wajibu huo.

Je, kuna viwango vipi vya ubora vinavyowalinda watumiaji dhidi ya athari zisizojulikana za- RF/EME?

Tume ya kimataifa ya Ulinzi wa Mionzi isiyo na Madhara (ICNIRP) imeunda miongozo, ambayo inafafanua viwango vya ubora, vikwazo na ngazi ya marejeleo ambayo inahitajika ili kuhakikisha usalama wa umma kwa jumla dhidi ya athari mbaya za mionzi isiyo na madhara (Kadhalika, kwa sasa Kenya inakamilisha miongozo yake).

Je, ni kiwango gani cha mionzi inayohusishwa na simu za mkono na SAR ni nini?

Kiwango cha mionzi ya nguvu ya sumaku umeme katika simu ya mkono ambacho hufyonza na mwili hupimwa kulingana na Viwango vyake Maalum vya Ufyonzaji wa Kawi (SAR). Simu ya kawaida ya mkono ina SAR ya uzani 1.6/kilo, lakini zingine zina kiwango cha juu kama uzani 2.0/kilo, ambacho ni kiwango cha juu cha SAR kinachopendekezwa kwa simu ya mkono.

Viwango vya juu zaidi vinavyoruhusiwa kama inavyofanuliwa na ICNIRP ni pamoja na:

- Uzani 0.4/kilo kwa matumizi ya kazini (kutumiwa na watu wazima ambao hatari yao inaelezewa chini ya hali inayojulikana na kudhibitiwa na hatua sahihi za tahadhari);
- Uzani 0.08 /kilo ya umma kwa ujumla (inategemea umri na hali ya kiafya na sio chini ya vikwazo vilivyoelezewa hapo juu) Je, ni viwango gani vya mionzi vinavyohusishwa na Minara ya Mawasiliano ya Simu ?

Kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya simu - nchini Kenya, idadi ya Minara ya Mawasiliano ya Simu inayojengwa imeongezeka ili kusaidia upatikanaji wa mtandao wa simu. Mitandao mingine isiyo ya waya, kama ile inayoweza ufikiaji wa masafa ya mtandao (kama vile WLAN) nayo pia inaongezeka.

Utafiti wa hivi karibuni wa Shirika la Afya Duniani (WHO) umeonyesha kuwa hatari ya RF/EME inayosababishwa na Minara ya Mawasiliano ya Simu huanzia 0.002% hadi 0.2% kwa mujibu wa kiwango kinachoruhusiwa cha kimataifa cha kuonyesha kiwango cha juu. Hatari kama hiyo, ambayo pia inategemea ukaribu wa binadamu kwa Minara

ya Mawasiliano ya Simu na masuala mengine ya kimazingira kama hayo, inalinganishwa na hatari ya RF/EME inayosababishwa na radio au Runinga – Vipeperushi vya matangazo na kwa hivyo ni ya chini sana (takriban mara 1000 chini kuliko kiwango kinachoruhusiwa cha hatari) ili isilete tishio kwa afya ya binadamu

Zingatia: nguvu ya mionzi wa RF/EME ni kubwa zaidi kwa ukaribu wake na chanzo chake na hupungua haraka katika uhusiano wa moja kwa moja na masafa. Ufikiaji wa mtandao kwa ukaribu wa masafa na Minara ya Mawasiliano mara nyingi huzuiliwa kwa sababu ya kwamba ishara ya masafa ya redio inaweza kuzidi mipaka inayoruhusiwa ya hatari.

